# MACHAKOS UNIVERSITY

**University Examinations 2018/2019**

**SCHOOL OF HUMANITIES AND SOCIAL SCIENCES**

**DEPARTMENT OF LINGUISTICS AND LANGUAGES**

**APRIL SESSSION EXAMINATION FOR**

**BACHELOR OF EDUCATION (ARTS)**

**AKS 0104 : INTRODUCTION TO KISWAHILI LITERATURE**

**DATE: SCHOOL BASED** **TIME:**

**MAAGIZO :** JIBU SWALI LA **KWANZA** NA MENGINE MAWILI

1. a) Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali. (alama 20)

KUMEKUCHA KUCHILEO (Amana 1982 : 47 -48 )

Usigombe ni kelele , jogoo linapowika,

Ni ishara usilale , fanya hima kuamka,

Kulala sana ni ndwele , utazikosa Baraka,

Wahi wakati haraka.

Akujulisha wakati , wakati wa kazi yako,

Sikiza yake sauti , iwikapo kokoiko,

Yakwambia usiketi , fuata wajibu wako,

Kule riziki iliko.

Usiku ukisha kucha , achana na kusinzia,

Wenziyo tutakuacha , pekeyo utabakia,

Ubaki kuuma kucha , na kwingi kujijutia,

Huna wa kukugaia.

Riziki mutakosana , burangeti siporusha,
Amka silale tena , upate kujisafisha,
Umshukuru Rabana , kukupa tena maisha,
Hima kujitayarisha.

Tayari uache nyumba , uole siku ya leo,
Mkulima wende shamba , muhandisi na koleo,
Sote tuivute kamba , ya harambee tegemeo,
Kumekucha kuchileo!

**MASWALI:**

i) Eleza aina ya Shairi. (alama 2)

ii) Eleza maudhui yanayojitokeza katika Shairi. (alama 2)

iii) Tambua tamathali tatu katika Shairi. (alama 6)

iv) Changanua umbo la Shairi. (alama 4)

v) Fafanua idhini ya mwandishi wa Shairi uliyoisoma. (alama 6)

b) Eleza aina tano za Tamthilia huku ukitoa mifano mwafaka. (alama 10)

2. a) Fafanua vipera vya nyimbo katika jamii yako kwa kutoa mifano. (alama 10)

b) Jadili asili ya sanaa kwa kuzingatia mitazamo ifuatayo: (alama10)

i) mtazamo wa kidhaniifu.

ii) mtazamo wa kiyakinifu.

3. a) Eleza dhima ya hadithi katika jamii. (alama 10)

b) Fafanua aina zifuatazo za wahusika . (alama 10)

i) mhusika hasidi

ii) mhusika nguli

iii) mhusika bapa

iv) mhusika kinyango

v) mhusika msaidizi

4. a) Tathmini tofauti zilizopo kati ya Fasihi andishi na Fasihi simulizi. (alama 10)

   b) Tofautisha hadithi fupi na Riwaya ya Kiswahili. (alama 10)

5. a) Huku ukitoa mifano mwafaka kutoka kwa kazi ya Fasihi uliyoisoma fafanua aina kumi za tamathali. (alama 10)

   b) Changanua mambo yanayopelekea umbo la shairi. (alama 10)